JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MAKAMU WA RAIS

# Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu

## MUHTASARI MAHSUSI

## 2020 - 2025









Juni, 2020

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu

*Kwa Muktadha wa Mkataba wa Minamata Kuhusu Zebaki*

## 2020 – 2025


Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:
Katibu Mkuu,
Ofisi ya Makamu wa Rais,
Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba,
Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais,
S. L. P. 2502,
**DODOMA.**
Simu Na.: +255 26 2329006
Fax Na.: +255 26 2329007
Barua pepe: km@vpo.go.tz

## DIBAJI

Zebaki ni moja ya kemikali hatarishi inayosababisha athari kwa afya ya binadamu na mazingira Duniani. Kemikali hii hutumika kuchenjua dhahabu katika shughuli za wachimbaji wadogo. Tafiti zimeonesha kuwa wachimbaji wadogo wa dhahabu ni chanzo cha uchafuzi wa mazingira utokanao na matumizi ya Zebaki dunaiani. Aidha, Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki unaelekeza nchi wanachama kuandaa na kutekeleza Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu inatoa ajira za moja kwa moja kwa takriban watu milioni 1.2 na ajira zisizo za moja kwa moja kwa watu milioni 7.2 sawa na asilimia 13 ya idadi watu nchini. Tathmini ya hali ilivyo kwa sasa inaonesha kuwa wachimbaji wadogo wa dhahabu hutumia kiasi cha tani 13.2 – 24.4 ya Zebaki kwa mwaka. Hata hivyo, matumizi yasiyo salama ya Zebaki husababisha athari kwa afya ya binadamu na mazingira.

Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu (2020 - 2025) umeandaliwa kukidhi matakwa ya Mkataba wa Minamata unolenga kupunguza pale inapowezekana kuondosha matumizi ya Zebaki katika shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu. Vilevile, Mpango-Kazi unahamasisha matumizi ya teknolojia mbadala wa Zebaki ili kupunguza changamoto za kiafya, mazingira, kiuchumi na kijamii zitokanazo na matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo.

Utekelezaji wa Mpango-Kazi huu utachangia katika juhudi za taifa za kufikia malengo ya maendeleo endelevu hususan kupunguza umasikini, hifadhi ya mazingira na kulinda afya ya binadamu. Mafanikio ya utekelezaji wa Mpango-Kazi huu yanategemea ushiriki wa wadau wote muhimu na hivyo natoa rai kwa Wizara za kisekta, Taasisi, Sekta Binafsi, washirika wa maendeleo, Asasi zisizo za Kiserikali, vikundi vya wachimbaji wadogo na wanahabari kushiriki kikamilifu katika kutekeleza Mpango-Kazi huu.



Mussa Azzan Zungu
**Waziri wa Nchi**
**Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira**

## SHUKRANI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa shukrani za dhati kwa Mfuko wa Mazingira wa Dunia kupitia Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa kwa mchango wao wa kifedha na kitaalam uliofanikisha maandalizi ya Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu. Mafanikio ya maandalizi ya Mpango-Kazi huu ni matokeo ya juhudi za wadau na Taasisi mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyingine wanastahili pongezi kwa mchango wao uliowezesha kukamilisha kazi hii.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Prof. Simon Msanjila, Katibu Mkuu, Wizara ya Madini na Dkt. Zainab Chaula aliyekuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano wao katika maandalizi ya Mpango-Kazi huu.

Aidha, Napenda kutoa shukrani kwa timu ya wataalam ambayo iliunda Kikosi-Kazi cha Taifa kwa mchango wao wa kitaalam na juhudi kubwa walioionesha katika maandalizi ya Mpango-Kazi huu. Wajumbe wa Kikosi-Kazi wanatoka Taasisi zifuatazo: Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Madini; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC); Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA); Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST); Shirika la Madini la Taifa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Rasilimali za Madini - Dodoma; na Shirika lisilo la Kiserikali la AGENDA.

Vilevile, Natoa shukrani zangu kwa Naibu Katibu Mkuu *Balozi* Joseph E. Sokoine, Ofisi ya Makamu wa Rais; Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira, Bw. Faraja Ngerageza, Ofisi ya Makamu wa Rais; na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mazingira, Bi. Kemilembe Mutasa, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kuratibu na kusimamia maandalizi ya Mpango-Kazi huu.

Mwisho, tunawashukuru wadau wote ambao wameshiriki kutoa michango yao kwa namna moja ama nyingine katika kuandaa Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Mhandisi Joseph K. Malongo
**KATIBU MKUU**

## YALIYOMO

DIBAJI ........ iii
SHUKRANI ........ iv
YALIYOMO ........ v

1.0 UTANGULIZI ........ 1
1.1 Maelezo ya Awali ........ 1
1.2 Maandalizi ya Mpango-Kazi ........ 1

2.0 HALI ILIVYO KATIKA SEKTA YA WACHIMBAJI WADOGO ........ 3
2.1 Maelezo Mafupi kuhusu Sekta ya wachimbaji wadogo ........ 3
2.2 Maeneo ya Wachimbaji Wadogo Nchini ........ 3
2.3 Hatua za Uchimbaji na Uchenjuaji wa Dhahabu ........ 4
2.4 Takwimu za Uchimbaji na Uchenjuaji wa Dhahabu ........ 5
2.5 Sera na Sheria za Usimamizi wa Sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu. 7
2.6 Jumuiya za wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini ........ 8
2.7 Changamoto za Sekta ya Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu ........ 8
2.8 Juhudi za Serikali ........ 9

3.0 MALENGO NA SHABAHA YA MPANGO-KAZI ........ 10
3.1 Changamoto ........ 10
3.2 Lengo la Mpango-Kazi ........ 10
3.3 Malengo Mahsusi ........ 11
3.4 Shabaha Muhimu za Mpango-Kazi ........ 11

4.0 MKAKATI WA UTEKELEZAJI ........ 12
**4.1 MKAKATI ........ 12**
4.1.1 Mkakati wa Kuondosha Mbinu Zisizofaa ........ 12
4.1.2 Mkakati wa tathmini ya Hali Halisi ya Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo ........ 12
4.1.3 Mkakati wa Kurasmisha Sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu ........ 12
4.1.4 Mkakati wa Kupunguza uchafuzi wa mazingira utokanao na Zebaki kwenye hewa, ardhi na maji. ........ 13
4.1.5 Mkakati wa kusimamia Biashara ya Zebaki ........ 13
4.1.6 Mkakati ya Kushirikisha wadau katika kutekeleza Mpango-Kazi ........ 13
4.1.7 Mkakati wa afya ya jamii wa kudhibiti na kukabiliana na madhara ya Zebaki kwa afya ya binadamu ........ 13
4.1.8 Mkakati wa kudhibiti athari za Zebaki kwa makundi yaliyo hatarini hususan watoto na wanawake wenye umri wa kuzaa. ........ 14
4.1.9 Mkakati wa kutoa taarifa na kuelimisha wachimbaji wadogo wa dhahabu 14

**4.2 MPANGO-KAZI WA UTEKELEZAJI ........ 15**
4.2.1 Mpango-Kazi wa Utekelezaji ........ 15
4.2.2 Gharama za Utekelezaji na Vyanzo vya Fedha ........ 23
4.2.3 Utaratibu wa Utekelezaji ........ 23

5.0 UTARATIBU WA TATHMINI NA UFUATILIAJI ........ 29
5.1 Ufuatiliaji ........ 29
5.2 Tathmini ya Utendaji ........ 29

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na.1: Majadiliano na vikundi mahsusi katika Mgodi wa Bingwa, Geita ........................ 2
Kielelezo Na. 2: Ramani ya Tanzania ikionesha Maeneo ya wachimbaji wadogo ...................... 4
Kielelezo Na.3: Hatua za Uchimbaji na Uchenjuaji wa Dhahabu............................................... 5
Kielelezo Na. 4: Shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu katika eneo la Kalole, Kahama, Shinyanga.......................................................................................................................... 6

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na.1: Makadirio ya kiasi cha Zebaki kinachotumika katika uchenjuaji wa dhahabu nchini.......................................................................................................................... 7
Jedwali Na. 2: Muhtasari wa Mpango-Kazi wa Utekelezaji katika kipindi cha 2020 - 2025...... 15
Jedwali Na 3: Majukumu ya kila madau katika kutekeleza Mpango-Kazi ................................ 23

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Maelezo ya Awali

Wachimbaji wadogo wa dhahabu wamekuwepo nchini zaidi ya miaka 100 iliyopita. Wachimbaji hawa wamekuwa wakiongezeka na kuchangia katika pato la taifa, ajira na ukuaji wa uchumi kwa wachimbaji kwa ujumla. Sekta hii inatoa ajira ya moja kwa moja kwa takriban watu milion 1.2 na ajira zisizo za moja kwa moja kwa watu milioni 7.2. Sekta hii pia inachangia asilimia (90) ya nguvukazi katika sekta ya madini nchini. Maeneo yenye historia ya muda mrefu katika uchimbaji mdogo wa dhahabu hapa nchini ni pamoja na Makongolosi na Itumbi (Chunya, Mbeya); Nyarugusu, Rwamgasa na Mgusu (Geita); Buhemba na Nyamongo (Mara); Noli (Dodoma); Londoni na Sekenke (Singida); na Nyangalata (Shinyanga).

Wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini hutumia kemikali ya Zebaki katika kuchenjua dhahabu. Tafiti zimebaini wachimbaji wadogo wa dhahabu kuwa chanzo kimojawapo cha uchafuzi wa mazingira utokanao na Zebaki duniani ambapo huchangia takriban asilimia 38 ya uchafuzi wa mazingira. Aidha, sekta hii ndio inayochangia uchafuzi wa mazingira kwa kiwango kikubwa kwa nchi zilizopo kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania.

Zebaki miongoni mwa vyanzo kumi (10) hatarishi kwa afya ya binadamu duniani kwa mujibu wa shirika la Afya Duniani. Katika kukabiliana na changamoto hii, jumuiya ya kimataifa ilipitisha Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki (2013) wenye madhumuni ya kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya uchafuzi utokanao na Zebaki.

Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi wanachama wa Mkataba huu inapaswa kuandaa na kutekeleza Mpango-Kazi wa kupunguza matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu kwa mujibu wa Ibara ya 7 ya Mkataba huo. Mpango-Kazi huu utakuwa ni wa miaka mitano kuanzia 2020 hadi 2025.

Matokeo tarajiwa ya utekelezaji wa Mpango-Kazi huu ni kupungua kwa uchafuzi wa mazingira unaotokana na Zebaki na hivyo kuchangia katika kuimarika kwa afya ya jamii, kuongeza uzalishaji wa dhahabu, kipato na ustawi wa wachimbaji wadogo na kuongeza mchango wa sekta hii katika uchumi wa Taifa.

## 1.2 Maandalizi ya Mpango-Kazi

Maandalizi ya Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu nchini ulianza Agosti 2016 na kukamilika Juni, 2020 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara za kisekta, Taasisi za Serikali, Asasi zisizo za Kiserikali, Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP).

Hatua za kuandaa Mpango-Kazi ni kama ifuatavyo:-

### *(i) Kikosi-Kazi cha Taifa*

Kikosi-Kazi cha Taifa kilianzishwa kwa uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ajili ya Kuandaa Mpango-Kazi husika na kilihusisha wajumbe kutoka Wizara za Kisekta, Taasisi za Serikali, Asasi zisizo za Kiserikali na vyuo vya elimu ya juu.

### *(ii) Tathmini ya hali ya wachimbaji wadogo wa dhahabu*

Tathmini ya hali ya wachimbaji wadogo wa dhahabu ilifanyika kati ya Januari, 2017 na Februari 2019 kwa kukusanya takwimu za hali ilivyo katika sekta ya wachimbaji wadogo ili kuweza kuandaa Mpango-Kazi. Mbinu zilizotumika katika kufanya tathmini husika ni pamoja na: kufanya mahojiano, majadiliano na vikundi mahsusi vya wachimbaji wadogo wa dhahabu **(Kielelezo**

**Na.1).** Jumla ya walengwa 372 walihojiwa ikiwa ni pamoja na viongozi wa Serikali, wachimbaji wadogo, wanawake na watoto.

Katika kufanya tathmini hiyo maeneo 40 ya wachimbaji wadogo wa dhahabu katika Mikoa tisa (9) ya Tanzania Bara ili kukusanya takwimu na kutambua changamoto za wachimbaji hao. Mikoa iliyotembelewa ni Geita, Shinyanga, Mbeya, Katavi, Mara, Tabora, Dodoma, Singida na Tanga. Tathmini ya hali ya wachimbaji wadogo wa dhahabu ilibaini masuala muhimu ambayo yalizingatiwa katika kuandaa Mpango-Kazi.



**Kielelezo Na.1**: Majadiliano na vikundi mahsusi katika Mgodi wa Bingwa, Geita

### *(iii) Ushirikishwaji wa wadau*

Mpango-Kazi uliandaliwa na kuwasilishwa katika vikao vya wadau vilivyofanyika Geita na Mbeya mwezi Aprili, 2019 kwa lengo la kupata maoni kuhusu Mpango-Kazi huu na ulipitishwa katika mkutano wa kitaifa wa wadau uliofanyika Jijini Dodoma.

# 2.0 HALI ILIVYO KATIKA SEKTA YA WACHIMBAJI WADOGO

## 2.1 Maelezo Mafupi kuhusu Sekta ya wachimbaji wadogo

Sekta ya wachimbaji wadogo ilianza kusimamiwa na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 ambapo utaratibu wa utoaji leseni kwa wachimbaji wadogo (*Primary Mining Licenses -PMLs*) ulianza. Kufuatia maendeleo na changamoto mbalimbali katika Sekta hii Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na Marekebisho yake ya mwaka 2017 zilifanyiwa maboresho ili kuimarisha utaratibu wa utoaji leseni za Uchimbaji mdogo wa madini.

Kufuatia maboresho mbalimbali katika sekta ya madini nchini kwa nyakati tofauti, kumekuwa na mafanikio makubwa ikiwemo kuongezeka kwa idadi ya leseni za uchimbaji zinazotolewa; uanzishwaji wa Shirikisho la Vyama vya wachimbaji wa Madini nchini ikiwa ni pamoja na Chama cha Wachimbaji Wanawake na Chama cha wafanyabiashara wa Madini; uanzishwaji wa masoko ya madini katika kila Mkoa; utengaji wa maeneo kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mdogo; na utoaji wa motisha za kiuchumi kama vile msamaha wa ushuru kwa wachimbaji wadogo.

Pamoja na mafanikio hayo, changamoto kadhaa zimejitokeza, ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo wa kitaasisi wa kutekeleza sheria na kanuni zilizopo; upatikanaji mdogo wa huduma za kifedha pamoja na mikopo; upatikanaji mdogo wa takwimu za kisayansi; na matumizi ya teknolojia duni za uchimbaji na uchenjuaji wa dhahabu.

## 2.2 Maeneo ya Wachimbaji Wadogo Nchini


Shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini zimejikita zaidi katika Mikoa ya Mara, Mwanza, Geita, Shinyanga, Tabora, Simiyu, Singida, Katavi, Mbeya, Tanga, Dodoma, Iringa, Lindi, Ruvuma, Morogoro na Songwe katika maeneo yapatayo 300. **(Kielelezo Na. 2).** Aidha, Mikoa ya kanda ya ziwa huchangia takribani asilimia 70 ya dhahabu yote inayozalishwa nchini ikifuatiwa na Mikoa ya Mbeya (Chunya) na Katavi (Mpanda).




Kielelezo Na. 2: Ramani ya Tanzania ikionesha Maeneo ya wachimbaji wadogo

### 2.3 Hatua za Uchimbaji na Uchenjuaji wa Dhahabu

Hatua muhimu katika uchimbaji na uchenjuaji wa Dhahabu kwa kutumia Zebaki zimeoneshwa katika **Kielelezo Na. 3**. Hii hujumuisha uchorongaji wa mwamba ili kupata mawe au udongo wenye dhahabu; kuponda mawe kwa mkono; kukausha kwenye jua mawe yaliyopondwa au udongo; kusaga kwa kutumia 'karasha'; uoshaji kwa kutumia maji kupata mchanga wenye dhahabu; uchejuaji wa mchanga kwa kutumia Zebaki ili kukamatisha dhahabu; na mwisho uchomaji wa mchanganyiko wa Zebaki na dhahabu ili kutenganisha dhahabu kwa kuwa Zebaki hugeuka mvuke na kuingia angani.




**Kielelezo Na.3: Hatua za Uchimbaji na Uchenjuaji wa Dhahabu**

## 2.4 Takwimu za Uchimbaji na Uchenjuaji wa Dhahabu

### *(i) Idadi ya Wachimbaji*

Sekta ya wachimbaji wadogo inatoa ajira za moja kwa moja kwa takriban watu milion 1.2 na ajira zisizo za moja kwa moja kwa watu milioni 7.2 sawa na asilimia 90 ya nguvu kazi katika sekta ya madini nchini. Wachimbaji wadogo walio wengi wana umri kati ya miaka 18 na 40 ambao hufanya shughuli zote za uchimbaji ikiwemo uchorongaji wa miamba na uchenjuaji wa dhahabu. Hali hii inaonesha kuwa watu wengi hujihusisha na shughuli za uchimbaji wa dhahabu katika umri mdogo. Aidha, idadi ya wanawake katika shughuli za uchimbaji mdogo ni kati ya asilimia 20 na 30 ya watu milioni 7.2 wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini **(Kielelezo Na.4)**.



**Kielelezo Na. 4:** Shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu katika eneo la Kalole, Kahama, Shinyanga

Vilevile, inakadiriwa kuwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 wapatao 10,000 wanajihusisha na shughuli za uchimbaji wa dhahabu nchini.

### *(ii) Upatikanaji na Biashara ya Zebaki*

Zebaki inayotumika katika shughuli za wachimbaji wadogo hapa nchini huingizwa kutoka nje ya nchi kupitia njia zisizo rasmi hususan kupitia mipaka ya Sirari na Namanga ambayo huingiza 55% ya Zebaki inayotumika nchini. Aidha, kupitia bandari bubu katika jiji la Dar es Salaam huchangia takriban 25% ya uingizaji wa Zebaki nchini; na 20% huingia kupitia mpaka wa Tunduma.

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani (2003), wafanyabiashara, mawakala na watumiaji wa Zebaki wanatakiwa kujisajili kwa Mkemia Mkuu wa Serikali.. Hata hivyo, hakuna taarifa za uingizaji, biashara na matumizi ya Zebaki zilizosajiliwa.

Kwa ujumla, biashara ya Zebaki katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu hufanywa kupitia maduka ya sonara na usambazaji wake huwafikia wachimbaji wadogo kupitia wamiliki wa leseni ndogo za uchimbaji wa madini, wanunuzi wa dhahabu na wamiliki wa mialo ya uchenjuaji wa dhahabu.

### *(iii) Matumizi ya Zebaki*

Uchenjuaji wa dhahabu hutumia takribani asilimia 80 ya Zebaki yote inayotumika nchini. Tathmini ya hali ilivyo inaonesha kuwa wachimbaji wadogo hutumia takribani tani 13.2 – 24.4 za Zebaki kwa mwaka **(Jedwali Na.1).** Mikoa inayoongoza katika matumizi ya Zebaki ni Geita, Mbeya, Shinyanga na Mara.

**Jedwali Na.1: Makadirio ya kiasi cha Zebaki kinachotumika katika uchenjuaji wa dhahabu nchini**

| Mkoa | Uzalishaji wa dhahabu (kg/mwaka) | Matumizi ya Zebaki (kg/mwaka) |
|---|---|---|
| Tabora | 695 | 1,112 |
| Singida | 655 | 1,048 |
| Mara | 554 | 886 |
| Geita | 2,800 | 4,480 |
| Mbeya | 1,159 | 1,854 |
| Katavi | 771 | 1,234 |
| Shinyanga | 910 | 1,456 |
| Dodoma | 414 | 662 |
| Tanga | 55 | 88 |
| Simiyu | 240 | 384 |
| Songwe | 472 | 755 |
| Morogoro | 267 | 427 |
| Iringa | 544 | 870 |
| Rukwa | 557 | 891 |
| Kigoma | 562 | 899 |
| Njombe | 670 | 1,072 |
| Ruvuma | 481 | 770 |
| Mwanza | 1,060 | 1,696 |
| Kagera | 1,150 | 1,840 |
| Lindi | 400 | 640 |
| Mtwara | 420 | 672 |
| Manyara | 425 | 680 |
| **JUMLA** | **15,261** | **24,416** |

## 2.5 Sera na Sheria za Usimamizi wa Sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu inasimamiwa na mfumo madhubuti wa Sera, Sheria na kitaasisi kwa kuzingatia mchango wake katika uchumi. Sera na Sheria zinazosimamia sekta hii ni kama ifuatavyo:

### *(i) Sera*

Sera ya Taifa ya Madini (2009) inalenga, pamoja na mambo mengine, kutambua, kusaidia na kuhamasisha uchimbaji endelevu wa madini ili kuongeza tija na mchango wa sekta ya wachimbaji wadogo katika uchumi na pato la Taifa kwa ujumla. Kwa upande mwingine, Sera ya Taifa ya Mazingira (1997) inatambua athari za kimazingira na kiafya zinazotokana na matumizi ya Zebaki katika shughuli za wachimbaji wadogo na hivyo kusisitiza usimamizi na udhibiti kemikali hiyo. Kadhalika, Sera ya Taifa ya Afya (2007) inalenga kuboresha sekta ya afya na ustawi wa watanzania kwa kuzingatia wale walio hatarini zaidi ikiwemo wachimbaji wadogo.

### *(ii) Sheria*

Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017 na 2019 inaweka utaratibu wa umilikishwaji wa maeneo kwa wachimbaji wadogo, utoaji leseni, uzingatiaji wa usalama katika shughuli za uchimbaji. Vilevile, Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali za Viwandani na Majumbani ya Mwaka 2003 inaelekeza udhibiti na usimamizi wa kemikali mbalimbali ikiwemo Zebaki. Aidha, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004

inaelekeza kufanya Tathmini ya Athari Kwa Mazingira (TAM) kwa wawekezaji na wachimbaji wa madini wakiwemo wachimbaji wadogo wa dhahabu.

### 2.6 Jumuiya za wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini

Wachimbaji wadogo wa dhahabu wanaendesha shughuli zao kupitia vyama ambavyo vimekuwepo kwa takribani miongo mitatu iliyopita na vinapatikana katika ngazi tofauti kuanzia ngazi ya Kitaifa, mkoa na maeneo ya uchimbaji wa dhahabu. Vyama hivi vinajikita zaidi katika kutoa misaada kwa wachimbaji wadogo na hivyo kushawishi mabadiliko ya kisera, kisheria na kiutendaji.

*(i) Ngazi ya Kitaifa na Mkoa*

Shirikisho la vyama vya wachimbaji wadogo nchini lilianzishwa Mwaka 1984 kwa lengo la kusimamia vyama vya wachimbaji vya mikoa na kuviunganisha Vyama hivyo na Serikali katika kuimarisha shughuli za uchimbaji wa madini. Aidha, vyama hivi vinawakilisha wachimbaji wadogo walio rasmi ambao idadi yao ni ndogo ikilinganishwa na wachimbaji wanaondesha shughuli zao bila leseni au vibali.

*(ii) Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo*

Baadhi ya wachimbaji wadogo katika maeneo mbalimbali wamejiunga na kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) ili kuweza kukusanya rasilimali fedha kwa ajili ya kununua vifaa, kupata leseni, kuimarisha utekelezaji wa shughuli zao. Vyama hivi vya Ushirika vipo katika baadhi ya maeneo ya wachimbaji kama vile Mgusu na Katente (Mkoa wa Geita) na Nyangalata (Shinyanga). Hata hivyo, maeneo mengi ya wachimbaji wadogo bado hayana vyama vya akiba na mikopo. Changamoto za uendeshaji wa vyama hivi ni ukosefu wa rasilimali fedha na utaalam.

*(iii) Chama cha Wafanya Biashara ya Madini Tanzania*

Chama cha wafanya Biashara ya madini Tanzania kilianzishwa mwaka 1990 kwa lengo la kuendeleza biashara ya madini kwa kushirikiana, kufanya tafiti, kuandaa na kushiriki maonesho ya madini ndani na nje ya nchi; kuongeza thamani ya madini; na kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo.

*(iv) Chama cha wachimbaji madini wanawake Tanzania*

Chama cha wachimbaji wanawake kilianzishwa Mwaka 1997 kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha, misaada ya kitaalam, teknolojia na masoko ili kuendeleza shughuli za uchimbaji wa madini zinazozingatia hifadhi na usimamizi wa mazingira.

### 2.7 Changamoto za Sekta ya Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu

Sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Matumizi ya njia zisizo salama katika uchenjuaji wa dhahabu kama vile uchomaji holela wa Zebaki unaohatarisha afya zao na uchafuzi wa mazingira;

(ii) Uchenjuaji wa Marudio yenye Zebaki kwa kutumia Sayanaidi ambako huchagiza zaidi uchafuzi wa mazingira;

(iii) Uelewa mdogo kuhusu madhara ya Zebaki;
(iv) Uelewa mdogo kuhusu mbinu salama za uchenjuaji;

(v) Madhara ya kiafya yanayosababishwa na kutokuzingatia kanuni za afya na usalama na ajali katika shughuli za uchimbaji wa dhahabu;

(vi) Kuchangia katika uharibifu wa mazingira hususan ukataji miti ovyo na uharibifu wa ardhi;

(vii) Baadhi ya wachimbaji wadogo kutozingatia sheria zinazosimamia sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu;

(viii) Uhaba wa taarifa za kijiolojia kwa wachimbaji wadogo kunakopunguza tija katika uzalishaji wa dhahabu; na

(ix) Uhaba wa huduma za kifedha katika baadhi ya maeneo ya wachimbaji wadogo.

Pamoja na changamoto hizi, sekta hii imeendelea kuwa sekta muhimu katika uchumi wa nchi kwa kutoa ajira kwa watu wengi.

## 2.8 Juhudi za Serikali

Katika kuhakikisha sekta ndogo ya wachimbaji wa dhahabu inawanufaisha wachimbaji wenyewe na taifa kwa ujumla, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Kutunga sheria ya madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 na 2019 ambapo pamoja na mambo mengine Sheria hiyo imeweka masharti ya kusimamia na kuendeleza sekta ndogo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu;

(ii) Uanzishaji wa Tume ya Madini na uboreshaji wa maabara ya Wakala wa Jiolojia Tanzania(GST) na Chuo cha Madini Dodoma(MRI);

(iii) Uanzishaji vituo mahiri saba (7) vya uchimbaji na uchenjuaji katika mikoa ya Kagera, Simiyu, Mara, Katavi, Ruvuma na Tanga; na mgodi wa mfano uliopo Rwamgasa katika Mkoa wa Geita;

(iv) Mafunzo ya njia bora za uchimbaji na uchenjuaji yalitolewa kwa wachimbaji zaidi 10,000 kwa muda wa miaka 5 (2013-2017); na

(v) Utoaji wa ruzuku kiasi cha bilioni 7 kwa wachimbaji wadogo wenye leseni katika vikundi 111.

## 3.0 MALENGO NA SHABAHA YA MPANGO-KAZI

### 3.1 Changamoto

Shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu zimekuwepo nchini kwa zaidi ya miaka 100. Tathmini inaonesha kuwa takribani tani 13.2 hadi 24.4 za Zebaki hutumika kwa mwaka katika shughuli za uchenjuaji wa dhahabu. Wachimbaji wadogo huchenjua dhahabu kwa kutumia mbinu ambazo huhatarisha afya ya binadamu na mazingira. Baadhi ya mbinu hizo ni pamoja na uchomaji holela wa dhahabu, uchenjuaji wa dhahabu karibu na maeneo ya makazi na vyanzo vya maji; na uchenjuaji wa marudio yenye Zebaki kwa kutumia Sayanaidi kunakochangia zaidi uchafuzi wa mazingira.

Upatikanaji na biashara ya Zebaki hapa nchini hutokana na uingizaji kutoka nje ya nchi kwa njia zisizo rasmi hususan kupitia mipaka ya Sirari na Namanga ambayo huingiza 55% ya Zebaki; bandari bubu katika jiji la Dar es Salaam huingiza takriban 25% ya Zebaki nchini; na mpaka wa Tunduma huingia 20%. Zebaki inayotumiwa na wachimbaji wadogo hupotea kwenye mazingira ambapo inakadiriwa kuwa asilimia 64 huingia ardhini na 36 huingia kwenye hewa wakati wa uchomaji. Hali hii huchangia uchafuzi wa mazingira unaotokana na Zebaki katika mazingira.

Tafiti kadhaa zimefanyika katika maeneo mbalimbali ya wachimbaji wadogo wa dhahabu, zimebainisha athari za Zebaki kwa afya ya binadamu na mazingira. Kulingana na matokeo ya tafiti hizo, inakadiriwa kuwa, asilimia 25 hadi 33 ya wachimbaji wadogo wa dhahabu hapa nchini wameathiriwa na Zebaki. Vilevile, tafiti hizo zimebaini kuwa baadhi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu kuwa na kiwango kikubwa cha Zebaki katika miili yao hadi mara 13 zaidi ya kiwango kinachokubalika na Shirika la Afya Duniani na hivyo kuashiria uwepo wa changamoto za kiafya zinazotokana na Zebaki katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Aidha, inakadiriwa kuwa takriban watoto 10,000 wanajihusisha na shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa dhahabu. Tafiti zinaonesha kuwa baadhi ya sababu zinazochangia ajira kwa watoto katika maeneo ya migodi ni pamoja na: hali ya umasikini; ukosefu wa msaada wa wazazi kutokana na hali ngumu ya maisha na talaka); shauku ya kutaka kuzisaidia familia zao hususan wale wanaotoka katika familia kubwa na wenye mzazi mmoja; wazazi kutoipa elimu kipaumbele; umbali mrefu wa kwenda shule; sababu za kimila kama vile baadhi ya mila zinawataka watoto kufanya kazi kama sehemu ya makuzi yao; mimba na ndoa za utotoni. Hivyo, matatizo ya kijamii na kiuchumi huchangia kwa kiasi kikubwa katika ajira za watoto.

Serikali kwa kushirikiana na wadau imechukua hatua mbalimbali za kusimamia sekta hii. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na: Kuhuisha masuala ya urasmishaji katika Sera ya Madini na Sera za sekta, kutungwa kwa Sheria mbalimbali zinazolenga kusimamia sekta hii, kuandaa na kutekeleza miradi mbalimbali inayolenga kutatua changamoto za wachimbaji wadogo; kuanizshwa kwa vituo mahiri vya uchenjuaji wa dhahabu na kujenga uwezo wa vyama vya wachimbaji wadogo ili kuimarisha ustawi wa wachimbaji hao. Hivyo, utekelezaji wa mikakati mahsusi ya Mpango-Kazi huu utachangia kukabiliana na baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya wachimbaji wadogo ili kulinda afya ya binadamu na uchafuzi wa mazingira

### 3.2 Lengo la Mpango-Kazi

Lengo la Mpango-Kazi huu ni kupunguza, na pale inapowezekana, kuondosha matumizi ya Zebaki katika shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu ili kulinda afya ya binadamu na mazingira.

### 3.3 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya Mpango-kazi huu ni:

i) Kupunguza matumizi ya Zebaki katika sekta ya Wachimbaji wadogo wa dhahabu kwa 30% na kukuza uelewa wa jamii ifikapo 2025;

ii) Kuimarisha mfumo wa kisheria, uwezo wa kitaasisi na ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi wa sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu ifikapo 2025; na

iii) Kuandaa na kutekeleza mkakati mahsusi wa kulinda afya ya jamii dhidi ya madhara ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu ifikapo 2025.

### 3.4 Shabaha Muhimu za Mpango-Kazi

Mpango-Kazi huu, unatarajia kufikia shabaha muhimu ambazo ni:-

i) Kupunguza uchomaji holela wa Zebaki, pamoja na kutumia teknolojia rafiki kwa mazingira za uchenjuaji wa dhahabu ifikapo 2025;

ii) Kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazosimamia uchimbaji madini, uhifadhi wa mazingira, afya ya jamii na ajira ifikapo 2025;

iii) Kuzijengea uwezo Wizara na Taasisi zenye dhamana ya Madini, Mazingira na Afya ifikapo 2025;

iv) Kuandaa na kutekeleza mkakati mahsusi wa kulinda afya ya Jamii dhidi ya madhara ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu ifikapo 2025;

v) Kujenga uwezo kwa angalau asilimia 20 ya wanawake wanaojishughulisha na uchimbaji wa dhahabu kifedha, teknolojia na mafunzo ifikapo 2025;

vi) Kuondosha ajira kwa watoto angalau asilimia 70 ya wanaofanya shughuli za uchimbaji wa dhahabu ifikapo 2025;

vii) Kuhakikisha angalau asilimia 40 ya Mipango ya Uhifadhi wa Mazingira inatekelezwa na wenye leseni za uchimbaji mdogo wa madini ya Dhahabu ifikapo 2025;

viii) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo nafuu kwa angalau asilimia 30 ya wachimbaji wadogo wa dhahabu ifikapo 2025;

ix) Kuanzisha na kuendesha masoko ya madini ya mikoa ili kuwawezesha wachimbaji kufikia kwa urahisi masoko ya dhahabu ifikapo 2025; na

x) Kujenga uwezo kwa vyama vya wachimbaji wa dhahabu vya kitaifa na mikoa ifikapo 2025.

## 4.0 MKAKATI WA UTEKELEZAJI

### 4.1 MKAKATI

Utekelezaji wa shughuli za Mpango-Kazi huu utashirikisha wadau mbalimbali. Aidha, mikakati mahususi ya kupunguza na pale inapowezekana kuondosha matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji wadogo ni kama ifuatavyo:-

#### 4.1.1 Mkakati wa Kuondosha Mbinu Zisizofaa

Mbinu zisizofaa ni pamoja na uchomaji holela wa dhahabu na uchenjuaji wa marudio *(mercury-contaminated tailings)* yenye Zebaki kwa kutumia Sayanaidi kunakochangia zaidi uchafuzi wa mazingira. Shughuli mahsusi za kuondosha mbinu zisizofaa kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu zinalenga kupunguza matumizi holela ya Zebaki na kuelimisha wachimbaji wadogo na jamii kwa ujumla kuhusu madhara ya Zebaki. Shughuli hizo ni pamoja na: -

i) Kuandaa na kutekeleza mpango wa kukuza uelewa na kutoa mafunzo kuhusu mbinu bora za udhibiti wa Zebaki wakati wa uchenjuaji;

ii) Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha na utaalam kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu ili kuhamasisha mbinu bora za matumizi ya Zebaki na teknolojia za uchenjuaji wa dhahabu zisizotumia Zebaki;

iii) Kuhamasisha tafiti na kueneza teknolojia mbadala zisizotumia Zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu; na

iv) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia bora na rahisi kwa ajili ya kuondosha Zebaki kwenye marudio yanayozalishwa na sekta ndogo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.

#### 4.1.2 Mkakati wa tathmini ya Hali Halisi ya Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo

Shughuli mahsusi zitakazotekelezwa katika kufanya tathmini ya hali halisi ya matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo ni pamoja na: -

i) Kuanzisha Kikosi-Kazi cha wadau kwa ajili ya kukusanya takwimu na kukipatia mafunzo mahsusi; na
ii) Kuanzisha na kuendesha kanzidata za kisekta zenye taarifa za Zebaki zinazohusiana na sekta za Afya, Mazingira, Madini na Ajira

#### 4.1.3 Mkakati wa Kurasmisha Sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu

Urasmishaji wa sekta ya wachimbaji wadogo ni hatua muhimu katika kuwezesha sekta hii ichangie pato la taifa na uchumi wa wachimbaji wadogo. Aidha, hatua hii itawezesha kuendesha shughuli za uchimbaji kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira. Shughuli mahsusi zitakazowesha kurasimisha sekta ya wachimbaji wadogo ni pamoja na:-

i) Kuandaa, kufanya mapitio na kusimamia utekelezaji wa sheria zinazosimamia na kudhibiti Zebaki ikiwemo kuandaa kanuni za usimamizi wa Zebaki;
ii) Kuimarisha utekelezaji sheria za mazingira, Ajira na Madini zinazopiga marufuku ajira kwa watoto katika shughuli ya Uchimbaji mdogo wa dhahabu;

iii) Kujenga uwezo wa taasisi zenye dhamana ya utoaji leseni na usimamizi wa sekta ndogo ya wachimbaji wa dhahabu ili kuwezesha urasimishaji wa sekta hiyo;
iv) Kuimarisha masoko ya madini vya mikoa ili kuhamasisha upatikanaji wa masoko ya dhahabu;
v) Kuainisha maeneo na kufanya utafiti wa kijiolojia ilikuwezesha kutenga maeneo mahsusi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu. Kujenga uwezo wa vyama vya wachimbaji wadogo wa dhahabu; na
vi) Kujenga uwezo wa vyama vya wachimbaji wadogo wa dhahabu

### 4.1.4 Mkakati wa Kupunguza uchafuzi wa mazingira utokanao na Zebaki kwenye hewa, ardhi na maji.

Katika kupunguza uchafuzi wa mazingira utokanao na Zebaki kwenye hewa, ardhi na maji Shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

i) Kuimarisha utekelezaji na uzingatiaji wa sheria za: usimamizi wa mazingira na mipango ya matumizi ya ardhi kudhibiti matumizi ya Zebaki katika maeneo lindwa;

ii) Kufanya ufuatiliaji wa uchafuzi wa mazingira (udongo, maji, hewa na vyakula) unaotokana na Zebaki katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu; na

iii) Kuandaa na kutekeleza mpango wa mawasiliano kwa umma kuhusu madhara ya kiafya yanayotokana na Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.

### 4.1.5 Mkakati wa kusimamia Biashara ya Zebaki

Mkakati huu utahusisha utekelezaji wa shughuli zifuatazo:-
i) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa kanuni za usimamizi na udhibiti wa Zebaki.
ii) Kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika kudhibiti na kufuatilia biashara ya Zebaki nchini
iii) Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika udhibiti wa biashara ya Zebaki.

### 4.1.6 Mkakati ya Kushirikisha wadau katika kutekeleza Mpango-Kazi

Utekelezaji wa Mkakati wa kushirikisha wadau utahusisha shughuli zifuatazo:
i) Kushirikisha wadau katika kutekeleza Mpango-Kazi;
ii) Kuimarisha ushirikiano baina ya wadau katika masuala yanayohusu sekta ya wachimabji wadogo wa dhahabu.

### 4.1.7 Mkakati wa afya ya jamii wa kudhibiti na kukabiliana na madhara ya Zebaki kwa afya ya binadamu

Ili kudhibiti na kukabiliana na madhara ya Zebaki kwa afya binadamu shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

i) Kuandaa na kutekeleza mpango jumuishi wa kukusanya takwimu za madhara ya Zebaki kwa afya ya jamii katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu;
ii) Kuandaa na kutekeleza mpango wa mafunzo kwa wataalam wa afya ili kuwajengea uwezo katika kufanya uchunguzi, utambuzi na tiba ya madhara ya Zebaki;

iii) Kuandaa na kusambaza miongozo ya kufanya uchunguzi na kutoa tiba ya magonjwa yanayotokana na Zebaki;
iv) Kuanzisha na kuimarisha vituo vya afya hususani vilivyopo katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu ili kukabiliana na magonjwa yanayo sababishwa na Zebaki; na
v) Kuandaa na kutekeleza mpango wa elimu kwa umma kuhusu madhara ya kiafya yanayotokana na shughuli za uchimbaji mdogo wa dhahabu.

### 4.1.8 Mkakati wa kudhibiti athari za Zebaki kwa makundi yaliyo hatarini hususan watoto na wanawake wenye umri wa kuzaa.

Ili kuweza kuzuia na kudhibiti madhara kwa makundi yaliyo katika hatari ya kuathiriwa na matumizi ya Zebaki katika shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu. Shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

i) Kuimarisha usimamizi wa sheria za mazingira, kazi na madini na Kanuni zake zinazozuia ajira za watoto katika uchimbaji mdogo wa dhahabu;

ii) Kuandaa na kutekeleza mipango ya uwezeshaji wa kifedha, teknolojia na mafunzo kwa wanawake katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu;

iii) Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kukuza uelewa kuhusu madhara ya Zebaki kwa wanawake wenye umri wa kuzaa mtoto na watoto katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu; na
iv) Kujumuisha masuala ya ajira kwa watoto katika mipango ya uendelezaji wa sekta wachimbaji wadogo wa dhahabu.

### 4.1.9 Mkakati wa kutoa taarifa na kuelimisha wachimbaji wadogo wa dhahabu

Changamoto zinazochangia uelewa mdogo kwa wachimbaji wadogo ni pamoja na: uhaba wa mifumo wezeshi ya kutoa taarifa; na ukosefu wa programu maalum za kuwezesha upatikanaji wa taarifa zinazohusu wachimbaji wadogo wa dhahabu. Ili kufikisha ujumbe na kuwezesha upatikanaji wa taarifa, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

i) Kuandaa na kutekeleza mpango wa kukuza uelewa kwa jamii zilizoathiriwa na Zebaki katika mikoa yenye wachimbaji wadogo wa dhahabu;
ii) Kuanzisha na kuendesha kanzidata za kisekta zenye taarifa za Zebaki zinazohusiana na sekta za Afya, Mazingira, Madini na Ajira;
iii) Kuandaa na kutekeleza mpango wa kukuza uelewa na kutoa mafunzo kuhusu mbinu bora za udhibiti wa Zebaki wakati wa uchenjuaji.
iv) Kuandaa na kutekeleza mpango wa kukuza uelewa kuhusu madhara ya Zebaki kwa Wanahabari.

## 4.2 MPANGO-KAZI WA UTEKELEZAJI

### 4.2.1 Mpango-Kazi wa Utekelezaji

Jedwali Na 4-2 linaonesha malengo, mikakati na utaratibu wa utekelezaji wa Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji wadogo wa dhahabu.

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Mpango-Kazi wa Utekelezaji katika kipindi cha 2020 - 2025**

| KAZI | VIASHIRIA | WAHUSIKA | MUDA WA UTEKELEZAJI (MWAKA) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| **Lengo Mahsusi 1: Kupunguza matumizi ya Zebaki katika sekta ya Wachimbaji wadogo wa Dhahabu kwa 30% na kukuza uelewa wa jamii ifikapo mwaka 2025.** | | | | | | | |
| 1.1 Kukuza uelewa na kutoa mafunzo kuhusu mbinu bora za udhibiti wa Zebaki katika uchenjuaji wa Dhahabu. | • Idadi ya wachimbaji walioelimishwa na wanaotumia mbinu bora za uchenjuaji wa dhahabu<br>• Idadi ya wachimbaji waliopata mafunzo | Wizara yenye dhamana ya Madini; NEMC; Chuo cha Madini; STAMICO; Tume ya Madini; Vyama vya wachimbaji wadogo; Asasi Zisizo za Kiserikali; na Vyombo vya Habari. | | | | | |
| 1.2 Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha na utaalam kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu ili kuhamasisha mbinu bora za matumizi ya Zebaki na teknolojia za uchenjuaji wa dhahabu zisizotumia Zebaki. | • Kiasi cha pesa kilichotengwa na kutumika<br>• Idadi wa wachimbaji waliowezeshwa kifedha<br>• Idadi ya taasisi za kifedha zinazotoa huduma za kifedha kwa wachimbaji | Wizara zenye dhamana ya: Madini, Fedha na Mipango; Benki Kuu ya Tanzania; NEMC; Chuo cha Madini; STAMICO; Tume ya Madini; Vyama vya Wachimbaji wadogo; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |

| KAZI | VIASHIRIA | WAHUSIKA | MUDA WA UTEKELEZAJI (MWAKA) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 1.3 Kuhamasisha tafiti na kueneza teknolojia mbadala zisizotumia Zebaki katika uchenjuaji wa Dhahabu. | • Idadi ya tafiti za teknolojia mbadala | Wizara yenye dhamana ya Madini; Tume ya Sayansi na Teknolojia; Taasisi za Utafiti; STAMICO; Tume ya Madini; Chuo cha Madini; TIRDO; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |
| 1.4 Kuwezesha uendeshaji wa vituo sita mahiri vya uchenjuaji wa dhahabu vilivyopo mikoa ya Mara, Kagera, Katavi, Mbeya, Ruvuma na Tanga; na mgodi wa mfano wa mafunzo uliopo Rwamgasa (Mkoa wa Geita) | • Idadi ya vituo vya mafunzo ya uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo<br>• Idadi ya wachimbaji waliopewa mafunzo kwenye vituo mahili vya uchenjuaji dhahabu | Wizara yenye dhamana ya Madini; STAMICO; Tume ya Madini; Wakala wa Jiolojia Tanzania; Taasisi za Elimu ya Juu; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |
| 1.5 Kuhamasisha matumizi ya teknolojia bora na rahisi kwa ajili ya kuondosha Zebaki kwenye marudio yanayozalishwa na sekta ndogo ya wachimbaji wadogo wa Dhahabu. | • Kiasi cha Zebaki kilichoondolewa kwenye marudio<br>• Idadi ya tecknolojia bora na rahisi za kuondosha Zebaki kwenye marudio | Wizara yenye dhamana ya Madini; NEMC; Chuo cha Madini; STAMICO; Tume ya Madini; Vyama vya wachimbaji wadogo; Taasisi za Elimu ya Juu; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |
| 1.6 Kuunda na kutoa mafunzo kwa Kikosi-Kazi cha Taifa kwa ajili ya kukusanya takwimu kuhusu matumizi na biashara ya Zebaki nchini. | • Idadi ya takwimu za kitaifa zilizokusanywa<br>• Idadi ya wataalamu waliopatiwa mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za matumizi ya Zebaki | Wizara zenye dhamana ya: Mazingira, Madini na Afya; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu; NEMC; Tume ya Madini; Chuo cha Madini; STAMICO, Vyama vya wachimbaji wadogo; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |

| KAZI | VIASHIRIA | WAHUSIKA | MUDA WA UTEKELEZAJI (MWAKA) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 1.7 Kukusanya takwimu kuhusu biashara na matumizi ya Zebaki katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu kila mwaka | • Idadi ya takwimu za kitaifa zilizokusanywa | Wizara zenye dhamana ya: Madini, Afya, Mambo ya Ndani na Mazingira; NEMC; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu; Chuo cha Madini; STAMICO; Vyama vya Wachimbaji wadogo; Tume ya Madini; Mamlaka ya Mapato Tanzania; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |
| 1.8 Kukuza uelewa kwa jamii zinazoathiriwa na Zebaki katika mikoa yenye wachimbaji wadogo wa Dhahabu | • Idadi ya vikundi vilivyoelimishwa<br>• Idadi ya mikoa iliyopata mafunzo<br>• Idadi ya wachimbaji wadogo | Wizara zenye dhamana ya: Madini, Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI; NEMC; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu; OSHA; Chuo cha Madini; STAMICO; Tume ya Madini; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |
| 1.9 Kuanzisha na kuendesha kanzidata za kisekta zenye taarifa za matumizi ya Zebaki katika sekta za Afya, Mazingira, Madini na Ajira. | • Kanzidata ya taarifa za matumizi ya Zebaki na afya katika jamii ya wachimbaji wadogo wa dhahabu | Wizara zenye dhamana ya: Afya, Madini, Ajira na Mazingira; NEMC; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu; OSHA; Chuo cha Madini; STAMICO; Tume ya Madini; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |

| KAZI | VIASHIRIA | WAHUSIKA | MUDA WA UTEKELEZAJI (MWAKA) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 1.10 Kukuza uelewa kuhusu madhara ya Zebaki kwa Wanahabari. | • Idadi ya wanahabari walioelimishwa<br>• Idadi ya Programu za uelimishaji umma kuhusu madhara ya Zebaki zilizotekelezwa<br>• Idadi ya Taarifa kuhusu uchafuzi wa mazingira (udongo, maji, hewa na vyakula) | Wizara zenye dhamana ya: Madini, Afya na Mazingira; Idara ya Habari - MAELEZO; Tume ya Madini; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu; STAMICO; NEMC; Taasisi za Utafiti na Elimu ya Juu; Vyama vya Wachimbaji wadogo; Baraza la Habari Tanzania; Asasi Zisizo za Kiserikali | | | | | |
| **Lengo Mahsusi 2: Kuimarisha mfumo wa kisheria, uwezo wa kitaasisi na ushirikishwaji wa wadau wa usimamizi wa sekta ndogo ya Wachimbaji Dhahabu ifikapo 2025** | | | | | | | |
| 2.1 Kuimarisha utekelezaji sheria za Hifadhi ya Mazingira, Ajira na Madini zinazopiga marufuku ajira kwa watoto katika shughuli ya Uchimbaji mdogo wa Dhahabu. | Idadi ya Sheria zilizotekelezwa | Wizara zenye dhamana ya: Ajira, Madini, Afya na TAMISEMI; NEMC; Tume ya Madini; Vyama vya wachimbaji wadogo; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |
| 2.2 Kuimarisha uwezo wa taasisi zenye dhamana ya usimamizi wa sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu ili kuendelea kuwezesha urasimishaji wa sekta hiyo. | Idadi ya taasisi zilizoimarishwa | Wizara zenye dhamana ya: Madini, Afya, Ajira, Mazingira; NEMC; STAMICO; OSHA; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu; na Tume ya Madini. | | | | | |
| 2.3 Kuwezesha uendeshaji wa masoko ya madini ya mikoa ili kurahisisha upatikanaji wa masoko ya dhahabu. | Idadi ya masoko ya dhahabu yaliyowezeshwa na kuimarishwa | Wizara zenye dhamana ya: Madini, Fedha; Tume ya Madini; STAMICO; Mamlaka ya Serikali za Mitaa Vyama vya wachimbaji wadogo | | | | | |

| KAZI | | VIASHIRIA | WAHUSIKA | MUDA WA UTEKELEZAJI (MWAKA) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 2.4 | Kuainisha maeneo na kufanya utafiti wa kijiolojia ili kuwezesha kutenga maeneo mahsusi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu. | Idadi ya maeneo yalifanyiwa utafiti wa kijiolojia | Wizara zenye dhamana ya: Ardhi na Madini; GST; STAMICO; Tume ya Madini; na Mamlaka za Serikali za Mtaa. | | | | | |
| 2.5 | Kuimarisha uwezo wa vyama vya wachimbaji wadogo wa dhahabu | Idadi ya vyama vya wachimbaji wadogo walioimarishwa | Wizara zenye dhamana ya: Madini, TAMISEMI; NEMC; STAMICO; Tume ya Madini; Vyama vya Wachimbaji wadogo; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |
| 2.6 | Kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika kudhibiti na kufuatilia biashara ya Zebaki nchini | Idadi ya Taasisi zilizoimarishwa | Wizara zenye dhamana ya: Madini na Mambo ya Ndani; TRA; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu; STAMICO; Tume ya Madini; na Vyama vya wachimbaji wadogo. | | | | | |
| 2.7 | Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika udhibiti wa biashara ya Zebaki. | • Idadi ya wafanyabiashara na mawakala wa Zebaki<br>• Kiasi cha Zebaki kilichoingizwa nchini | Wizara zenye dhamana ya: Mazingira, Mambo ya Nje, Mambo ya Ndani na Madini; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali; na Tume ya Madini. | | | | | |
| 2.8 | Kuanzisha na kuendesha kongamano la wadau wa sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu kila mwaka | • Idadi ya mikutano ya kitaifa ya wadau wa sekta ya madini<br>• Idadi ya washiriki katika makongamano ya kitaifa kuhusu wachimbaji wadogo | Wizara zenye dhamana ya: Madini na Mazingira; NEMC, Tume ya Madini; na Vyama vya wachimbaji wadogo. | | | | | |

| KAZI | | VIASHIRIA | WAHUSIKA | MUDA WA UTEKELEZAJI (MWAKA) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 2.9 | Kukusanya takwimu kuhusu madhara ya Zebaki kwa afya ya jamii katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu | Idadi ya takwimu za kitaifa zilizokusanywa kuhusu madhara ya Zebaki | Wizara zenye dhamana ya: Afya, Madini na TAMISEMI; OSHA; Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali; NIMR; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi za Utafiti; Vyama vya wachimbaji wadogo; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |
| **Lengo Mahsusi 3: Kuandaa na kutekeleza mkakati mahsusi wa kulinda afya ya jamii dhidi ya madhara ya Zebaki kwa jamii ya wachimbaji wadogo wa dhahabu ifikapo 2024** | | | | | | | | |
| 3.1 | Kutoa mafunzo kwa wataalam wa afya ili kuwajengea uwezo katika kufanya uchunguzi, utambuzi na tiba kwa walioathiriwa na Zebaki | • Idadi ya vifaa tiba vilivyonunuliwa kwa ajili ya kufanya utambuzi na uchunguzi<br>• Idadi ya Programu za uelimishaji umma kuhusu madhara ya Zebaki zilizotekelezwa | Wizara zenye dhamana ya: Afya na TAMISEMI; NIMR; OSHA; na Taasisi za Elimu ya Juu. | | | | | |
| 3.2 | Kuandaa na kusambaza miongozo ya kufanya uchunguzi na kutoa tiba ya magonjwa yanayotokana na kuathiriwa na Zebaki | Idadi ya miongozo iliyoandaliwa | Wizara zenye dhamana ya: Afya na TAMISEMI; GCLA; NIMR; na Taasisi za Utafiti na Elimu ya Juu. | | | | | |
| 3.3 | Kuanzisha na kuimarisha vituo vya afya hususani vilivyopo katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu ili kukabiliana na magonjwa yanayo sababishwa na Zebaki | Idadi ya vituo vya afya vilivyoimarishwa au kuanzishwa kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu | Wizara zenye dhamana ya: Afya, Fedha na TAMISEMI. | | | | | |

| KAZI | | VIASHIRIA | WAHUSIKA | MUDA WA UTEKELEZAJI (MWAKA) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 3.4 | Kuandaa na kutekeleza mkakati wa elimu kwa umma kuhusu madhara ya kiafya yanayotokana na shughuli za uchimbaji mdogo wa dhahabu | Idadi ya Programu za uelimishaji umma kuhusu madhara ya Zebaki zilizotekelezwa | Wizara zenye dhamana ya: Afya, Mazingira, Madini, TAMISEMI na Habari; OSHA; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu; Tume ya Madini; Chuo cha Madini; NEMC; NIMR; Taasisi za Utafiti na Elimu ya Juu; Vyama vya wachimbaji wadogo; Asasi Zisizo za Serikali; na Vyombo vya Habari. | | | | | |
| 3.5 | Kufanya uchunguzi na ufuatiliaji wa uchafuzi wa mazingira (udongo, maji, hewa na vyakula) unaotokana na Zebaki katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu | • Mpango wa ufuatiliaji wa uchafuzi wa mazingira (udongo, maji, hewa na vyakula).<br>• Idadi ya sampuli za mazingira zilizokusanywa<br>• Idadi ya Taarifa kuhusu uchafuzi wa mazingira (udongo, maji, hewa na vyakula) | Wizara zenye dhamana ya: Mazingira, Maji, Madini na Afya; Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu; NEMC; TBS; Taasisi za Utafiti; na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. | | | | | |
| 3.6 | Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano kwa Umma kuhusu madhara kwa afya na mazingira yanayotokana na Zebaki | Idadi ya Programu za uelimishaji umma kuhusu madhara ya Zebaki zilizotekelezwa | Wizara zenye dhamana ya: Afya, Madini, Mazingira na TAMISEMI; Mamlaka ya Maabaraya Mkemia Mkuu; NIMR; NEMC; STAMICO; OSHA; Tume ya Madini; Taasisi za Utafiti na Elimu ya Juu; Vyama vya wachimbaji wadogo; Asasi Zisizo za Kiserikali na Vyombo vya Habari. | | | | | |

| KAZI | | VIASHIRIA | WAHUSIKA | MUDA WA UTEKELEZAJI (MWAKA) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 3.7 | Kuwawezesha wanawake kwa kuwapatia fursa za mikopo, teknolojia na kutoa mafunzo katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu | • Idadi ya wanawake wanaojihusisha na uchimbaji na biashara mbalimbali katika maeneo ya wachimbaji wadogo<br>• Idadi ya jitihada za kuwawezesha wanawake ili kushiriki kwenye uchibaji mdogo wa dhahabu | Wizara zenye dhamana ya: Madini, Jinsia na TAMISEMI; Tume ya Madini; STAMICO; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Vyama vya Wachimbaji wadogo; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |
| 3.8 | Kukuza uelewa kuhusu madhara ya Zebaki kwa wanawake wenye umri wa kuzaa pamoja na watoto katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu | Idadi ya watoto na wanawake waliopatiwa elimu kuhusu madhara ya kiafya yatokanayo na madhara | Wizara zenye dhamana ya: Ajira, Madini, Afya, Mazingira na TAMISEMI; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Tume ya Madini; Vyama vya wachimbaji wadogo; Asasi Zisizo za Kierikali; na Vyombo vya Habari. | | | | | |
| 3.9 | Kujumuisha masuala ya ajira kwa watoto katika mipango ya uendelezaji wa sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu. | Idadi ya matukio yanayohusu ajira kwa watoto kwenye maeneo ya uchimbaji mdogo wa dhahabu | Wizara zenye dhamana ya: Ajira, Madini, Afya, Mazingira na TAMISEMI; Mamlaka za Serikali za Mtaa; Tume ya Madini; Vyama vya wachimbaji wadogo; na Asasi Zisizo za Kiserikali. | | | | | |

### 4.2.2 Gharama za Utekelezaji na Vyanzo vya Fedha

Jumla ya gharama za kutekeleza Mpango-Kazi ni dola za Marekani 14,400,000 kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia (2020 hadi 2025). Vyanzo vya fedha kwa ajili ya utekelezaji wake vinategemea mchango wa sekta binafsi, bajeti ya Serikali na washirika wa maendeleo ikiwemo Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF).

### 4.2.3 Utaratibu wa Utekelezaji

Utekelezaji wa Mpango-Kazi huu utashirikisha wadau mbalimbali ikiwemo Taasisi za Serikali, washirika wa maendeleao, sekta binafsi na Asasi zisizo za kiserikali. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Madini, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wataratibu utekelezaji wa Mpango-Kazi huu. Majukumu ya wadau wengine ni kama yanavyoonekana katika jedwali Na. 3.

**Jedwali Na 2: Majukumu ya kila madau katika kutekeleza Mpango-Kazi**

| Taasisi | Majukumu |
|---|---|
| 1. Ofisi ya Rais - TAMISEMI | • Kuratibu na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kijamii katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kuhamasisha elimu kwa umma kuhus athari za Zebaki kwa afya ya binadamu na mazingira. .<br>• Kujenga uwezo wa vyama vya wachimbaji wadogo wa dhahabu<br>• Kupunguza ajira kwa watoto katika shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kushirikiana na wadau wengine katika kusimamia hifadhi ya mazingira katika migodi ya wachimbaji wadogo. |
| 2. Ofisi ya Makamu wa Rais | • Kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Minamata na Mikataba mingine ya kimataifa na Kikanda ya hifadhi ya mazingira<br>• Kuratibu Utekelezaji wa Mpango-Kazi<br>• Kutoa elimu kwa umma na kujenga uwezo kuhusu masuala ya Zebaki.<br>• Kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004<br>• Kusimamia utekelezaji wa Kanuni za udhibiti na Usimamizi wa Zebaki.<br>• Kuandaa taarifa za hali halisi ya matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo<br>• Kuratibu upatikanaji wa rasilimali za kutekeleza Mpango-Kazi. |

| Taasisi | Majukumu |
|---|---|
| 3. Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na watu wenye ulemavu | • Kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Kazi kuhusu kuondosha ajira kwa watoto katika maeneo ya migodi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kuanzisha na kuendesha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za masuala ya kazi na ajira kwa watoto katika maeneo ya wachimbaji wadogo. |
| 4. Wizara ya Madini | • Kuratibu utekelezaji wa Mpango-Kazi;<br>• Kuhakikisha matumizi ya Zebaki yanapungua na pale inapowezekana yanaondoshwa katika migodi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu;<br>• Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Zebaki<br>• Kuratibu upatikanaji wa rasilimali fedha na kujenga uwezo wa kitaalamu katika kutumia mbinu bora za uchenjuaji wa dhahabu;<br>• Kuratibu na kuwezesha kufanyika kwa tafiti kuhusu mbadala wa Zebaki;<br>• Kusimamia uendeshaji wa vituo mahiri vya uchenjuaji wa dhahabu;<br>• Kuhamasisha matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira za kukamatisha Zebaki kutoka kwenye mabaki ya uchenjuaji;<br>• Kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya kijiolojia kwa ajili ya shughuli za uchimbaji wa madini;<br>• Kuandaa taarifa za hali ya matumizi ya Zebaki katika maeneo ya wachimbaji wadogo;<br>• Kujenga uwezo wa vyama vya wachimbaji wadogo wa dhahabu; na<br>• Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Madini. |
| 5. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. | • Kuandaa Mkakati wa Afya kwa umma wa kudhibiti athari za Zebaki kwa afya ya binadamu katika maeneo ya wachimbaji wadogo;<br>• Kuratibu utekelezaji wa Mpango-Kazi;<br>• Kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za Zebaki kwa afya ya binadamu.<br>• Kuratibu na kufanya ufuatailiaji wa uzingatiaji wa masuala ya afya kwa umma katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kusimamia utekelezaji wa Sheria zinazosimamia Afya ya Jamii na Mazingira.<br>• Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha na utaalam katika kutekeleza Mpango-Kazi. |
| 6. Wizara ya Katiba na Sheria | • Kuwezesha kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni mbalimbali za kudhibiti na kusimamia matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo<br>• Kutoa ushauri wa Kisheria kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Minamata na Mikataba mingine ya Kimataifa na Kikanda ya hifadhi ya mazingira. |

| Taasisi | Majukumu |
| --- | --- |
| 7. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | • Kuwezesha Tanzania kushiriki mikutano ya kikanda na kimataifa ya udhibiti na usimamizi wa Zebaki.<br>• Kuratibu majadiliano na wafadhili kwa ajili ya upatikanaji wa rasilimali fedha za kutekeleza Mpango-Kazi. |
| 8. Wizara ya Fedha na Mipango | • Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha za kutekeleza Mpango-Kazi.<br>• Kuwezesha Tanzania kulipia ada ya uanachama ya Mkataba wa Minamata na Mikataba mingine ya Kimataifa na Kikanda ya hifadhi na mazingira. |
| 9. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. | • Kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya wachimbaji wadogo<br>• Kuhamasisha elimu kwa umma kuhusu Mpango wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya wachimbaji wadogo.<br>• Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ardhi na Kanuni zake. |
| 10. Tume ya Madini | • Kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Madini na Kanuni zake.<br>• Kuelimisha umma kuhusu masuala ya Zebaki<br>• Kusimamia na kufuatilia uendeshwaji wa vituo mahiri vya uchejuaji wa dhahabu.<br>• Kusimamia uendeshaji wa masoko ya dhahabu.<br>• Kusimamia na kuwezesha urasmishaji wa sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu. |
| 11. Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali | • Kusajili, kudhibiti na kusimamia uingizaji nchini, usafirishaji na matumizi ya kemikali ikiwemo Zebaki chini ya Sheria ya udhibiti na usimamizi wa Kemikali za Viwandani na Majumbani ya Mwaka 2003<br>• Kuandaa taarifa za uingizaji na matumizi ya Zebaki nchini hususan kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Zebaki.<br>• Kutekeleza Mkakati wa afya ya jamii unaohusu udhibiti wa madhara ya Zebaki kwa afya ya binadamu katika maeneo ya wachimbaji wadogo.<br>• Kuanzisha kanzidata ya taarifa za madhara ya kiafya yatokanayo na Zebaki. |
| 12. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) | • Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni ya usimamizi wa Zebaki ya mwaka 2019.<br>• Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Zebaki.<br>• Kuhamasisha matumizi ya teknolojia rafiki na Salama. Kuanzisha kanzidata ya taarifa za usimamizi wa mazingira katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu. |

| Taasisi | Majukumu |
| --- | --- |
| | • Kujenga uwezo wa vyama vya wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kufanya Tathmini na ufuatiliaji wa uchafuzi utokanao na Zebaki katika maeneo ya wachimbaji wadogo.<br>• Kuratibu makongamo ya wadau wa mazingira katika sekta ya madini. |
| 13. Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) | • Kutekeleza Sheria ya Usalama na Afya mahali pa kazi ya Mwka 2003 na Kanuni zake.<br>• Kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za kiafya zitokanazo na matumizi ya Zebaki.<br>• Kuanzisha kanzidata ya taarifa za usalama na afya katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kutoa mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi katika maeneo ya wachimbaji wadogo. |
| 14. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | • Kuandaa taarifa ya uingizaji wa Zebaki nchini<br>• Kudhibiti uingizaji wa Zebaki nchini. |
| 15. Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) | • Kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kuhamasisha mbinu bora na teknolojia salama za uchenjuaji wa dhahabu.<br>• Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Zebaki<br>• Kuratibu tafiti za teknolojia mbadala wa Zebaki.<br>• Kuanzisha kanzidata ya taarifa za wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kurasimisha wachimbaji wadogo wa dhahabu. |
| 16. Chuo cha Madini (MRI) | • Kufanya tafiti za teknolojia mbadala wa Zebaki.<br>• Kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbadala wa Zebaki<br>• Kutoa elimu kwa umma kuhusu matokeo ya tafiti za teknolojia mbadala.<br>• Kutoa mafunzo ya uchimbaji endelevu na uchenjuaji wa dhahabu |
| 17. Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) | • Kuratibu na kusimamia tafiti za teknolojia mbadala wa Zebaki na kusambaza teknolojia husika katika maeneo ya wachimbaji wadogo. |
| 18. Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) | • Kukusanya takwimu za hali ya wachimbaji wadogo wa dhahabu<br>• Kuhuisha kanzidata za kisekta katika mfumo wa taifa wa takwimu. |
| 19. Wakala wa Jiolojia Tanzania (Geological Survey of Tanzania -GST) | • Kuainisha maeneo na kufanya utafiti wa kijiolojia ili kuwezesha kutenga maeneo mahsusi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kutoa elimu kwa umma kuhusu matokeo ya tafiti zilizofanyika na kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wachimbaji wadogo. |

| Taasisi | Majukumu |
|---|---|
| 20. Taasisi ya Taifa ya utafiti wa magonjwa ya Binadamu (NIMR) | • Kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya kuweza kutambua na kutibu magonjwa yatokanayo na madhara ya Zebaki.<br>• Kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara yakiafya yatokanayo na matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kufanya tafiti za magonjwa yanayotokana na shughuli za uchimbaji wa dhahabu. |
| 21. Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) | • Kufanya tafiti za teknolojia mbadala wa Zebaki na kusambaza teknolojia hizo katika maeneo ya wachimbaaji wadogo |
| 22. Idara ya Habari - MAELEZO | • Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Zebaki<br>• Kushirikiana na Wizara na Taasisi za kisekta kuandaa Mkakati wa elimu kwa umma kuhusu madhara ya Zebaki kwa afya ya biandamu na mazingira. |
| 23. Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs) | • Kutenga maeneo kwaajili ya shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kutambua na kutoa mikopo ili kuwezesha shughuli za wachimbaji wadogo.<br>• Kuondosha ajira kwa watoto katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kushirikiana na wadau katika kusimamia masuala ya hifadhi ya mazingira kwa wachimbaji wadogo.<br>• Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004. |
| 24. Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA) | • Kuelimisha jamii za wachimbaji wadogo kuhusu athari za Zebaki kwa watoto na mama wajawazito katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kushiriki kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya katika kufanya utambuzi na kutibu magonjwa yatokanayo na madhara ya Zebaki. |
| 25. Vyama vya wachimbaji wadogo (FEMATA, TAWOMA na WIMA) | • Kujenga uwezo na kuelimisha jamii ya wachimbaji wadogo kuhusu masuala ya Zebaki.<br>• Kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbadala wa Zebaki.<br>• Kushirikiana na wadau katika kuondosha ajira kwa watoto katika shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu. |
| 26. Asasi za Kiraia (CSOs) | • Kuelimisha jamii ya wachimbaji wadogo kuhusu masuala ya Zebaki na teknolojia mbadala.<br>• Kutekeleza Mkakati wa afya ya jamii unaohusu kujikinga na madhara ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu. |

| Taasisi | Majukumu |
|---|---|
| | • Kuhamasisha uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika shughuli za wachimbaji wadoogo wa dhahabu<br>• Kufanya tafiti za teknolojia mbadala wa Zebaki na kusambaza teknolojia husika kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu. |
| 27. Taasisi za Elimu na Utafiti | • Kufanya tafiti za teknolojia mbadala wa Zebaki na kusambaza teknolojia hizo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kufanya tafiti za hali ya matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.<br>• Kujenga uwezo wa kitaalamu kwa vyama vya wachimbaji wadogo kuhusu masuala ya Zebaki na teknolojia mbadala.<br>• Kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo kuhusu uchimbaji na uchenjuaji rafiki kwa mazingira kupitia vituo mahiri vya uchenjuaji wa dhahabu. |
| 28. Chama cha Wafanya biashara wa Madini (TAMIDA) | • Kujenga uwezo wa kitaalamu kwa vyama vya wachimbaji wadogo wa dhahabu<br>Kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbadala wa Zebaki |
| 29. Sekta Binafsi | • Kutoa mitaji na huduma za kifedha kwa ajili ya shughuli za uchenjuaji. . |
| 30. Vyombo vya Habari | • Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Zebaki na madhara ya kiafya yatokanayo na matumizi ya Zebaki |

## 5.0 UTARATIBU WA TATHMINI NA UFUATILIAJI

Sehemu hii inatoa utaratibu ufuatiliaji na tathmini kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2020 hadi 2025 ya utekelezaji wa Mpango-Kazi. Tathmini na ufuatiliaji wa mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa mkakati huu ni muhimu ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa. Ufuatiliaji wa utekelezaji na tathmini utafanyika kwa njia shirikishi na kwa msingi endelevu. Wizara za Kisekta na Taasisi zitatayarisha na kuwasilisha taarifa za shughuli zilizopangwa na kutekelezwa. Upimaji wa maendeleo ya utekelezaji wa mpango utategemea viashiria na vigezo mbalimbali vya utendaji vilivyowekwa.

### 5.1 Ufuatiliaji

Ufuatiliaji utahusisha Mfumo endelevu wa ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi na uandaaji wa taarifa. Hii itatoa taarifa/ kwa Wizara zenye dhamana ya: mazingira, madini na afya kwa kushirikiana na wadau wengine kuhusu hatua zinazoendelea kwa lengo la kutathmini kiwango cha utekelezaji wa mafanikio yaliyopatikana kulingana na malengo yaliyowekwa na matumizi ya fedha zilizotengwa.

### 5.2 Tathmini ya Utendaji

Tathmini ya utendaji itafanyika mara kwa mara kutambua ufanisi wa utekelezaji wa lengo la Mkakati. Aidha, tathmini ya utekelezaji itafanyika kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza itafanyika kila baada ya miaka miwili kwa ajili ya kupima maendeleo ya utekelezaji. Vilevile tathimni ya mwisho itafanyika kwa lengo la kupima mafanikio yaliyofikiwa kulingana na lengo la Mpango-Kazi.Viashiria vikuu katika ufanyaji wa tathmini hii ni kama vifuatavyo: matumizi ya teknolojia mbadala wa Zebaki; matumizi ya njia bora/mbinu salama za uchomaji wa dhahabu iliyokamatishwa na Zebaki *(gold amalgam)* na matumizi ya vigida (*mercury retorts).*